

Title: Under the Mango Trees

EPISODE 3

Author: Romie Singh

Editors: Susanne Fuchs, Katrin Ogunsade, Maja Braun

List of characters for episode 3:

- Narrator
- April
- Desirée
- Lorraine
- Endurance
- Granma
- Alice
- Eric
- Children in background

INTRO:

Karibu kwenye sehemu ya tatu ya mchezo kwa jina Chini ya Miembe, katika mfululizo wa hadithi ya kuisimua kwenye Noa Bongo Jenga maisha Yako. Leo hii Desirée anatarajia kupata taarifa zaidi kuhusu kifo cha mama yake kwani amepanga kumtembelea rafiki yake mpendwa Lorraine, wiki endi hii atakuwa pamoja pia na ndugu pacha wa Lorraine, Eric na mama yao ambae ni Daktari Alice. Lakini kabla ya kuanza safari yake anajaribu kumshawishi nyanya yake juu ya wazo lake, angependa sana mdogo wake Endurance, asaidie katika kufanya kazi za nyumbani.

SIG.TUNE UP HOLD UNDER AND FADE

NARRATOR: Nyumba ndogo iliyo shambani katika kijiji cha Mtelera imezunguukwa na miti ya miembe ambayo ilipandwa kila mti kwa wakati wake – kuashiria ukumbusho wa mtu Fulani mwananmume, mwanmke au mtoto aliyefariki katika ukoo wa Okoro . Hata hivyo dalili za uhai zilijaa tele kwenye nyumba ya nyanya Linda. Kulikuwa na watoto wadogo wanne ambao ni Binamu za – Desirée na Endurance – watoto hao walileta faraja katika nyumba ile ijapokuwa fujo zao zilimtia wazimu Desirée wakati mwingine. Hali hiyo ilmfanya afikirie kwamba mdogo wake Endurance alitumia sababu ya kuwa mwanamume ili asiwajibike na aina ya kazi yoyote pale nyumbani yaani hakutaka kusaidia hata kidogo.

Sc. 1 Morning in the kitchen

1. **SFX:** Distant cows/ chickens /birds. Cutlery. Sounds of children playing around, coming to the table, eating.

2. **DESIRÉE:** (angry) Endurance ana miaka13, nyanya. Itabidi anisaidie kufanya baadhi ya kazi za hapa nyumbani.

3. **ENDURANCE:** Tayari mimi naaidia nani anawapeleka ng’ombe malishoni kila siku saa kumi na

moja alfajiri 5? Nauliza ni nani dada mpendwa?

4. DESIRÉE: Ndio sikatai, wakati mimi ninapika, nafua na kupiga pasi nguo zote, nyanya, Lorraine anaweza kunisaidia niwe mwimbaji. Ameniambia kuhusu uchaguzi wa kushiriki kwenye mashindano makubwa hii ni bahati ya mara moja tu katika maisha.

5. GRANMA: Uchaguzi? Kuimba? Bah! Ni upuuzi gani msichana huyo wa mjini anajaribu kukushawishi?

6. ENDURANCE: Niliwasikia wakifanya mazoezi shuleni. (imitating) Oohhh...yeah...

7. DESIRÉE: Nyanya tafadhali usimsikilize! Sisi tunajua. Nafikiri mimi, naweza kuimba vizuri, na Lorraine ameniomba niende kwao wikiendi hii ili tukafanye mazoezi.

8. GRANMA: Na kazi za hapa je? hapana! hapana, Desirée. Mimi sina nguvu za

kuwaangalia watoto wanne pamoja na
Endurance .

9. DESIRÉE: Endurance ni mkubwa na anaweza kukusaidia nyanayais . dada Bella, alisema pia yeye anaweza kusaidia iwapo tutahitaji msaada wake. Angalia nyanya! Ninachoomba ni fursa hii moja peke yake hata kama sitofaulu lakini nitakuwa nimejaribu na wala sitopata hasara yoyote. Na kama una wasiwasi kwa sababu ya shule wala usihifi nyanya uchaguzi huu utafanyika wakati wa likizo.
10. GRANMA: Mimi nimesema hapana. Kwanza nafikiria hata hiyo shule yenyewe ungeiwacha tu, halafu utakuwa na wakati wa kutosha wa kutuhudumia sisi sote pamoja na huo muziki wako ikiwa kweli hilo ndilo ulitakalo.
11. DESIRÉE: Lakini shule ni muhimu. Vile vile huenda pia nisifaulu katika huo uchaguzi wenyewe labda sina uwezo wa kuwa mwanamuziki.
12. ENDURANCE: (sarcastic) Hiyo ni hakika huwezi!

13. DESIRÉE: Sawa lakini kwanza mpaka nijaribu, nione kama kweli hicho ndico kitu ninachotaka kukifanya maishani. Vinginenyo itabaki kama ndoto tu.
14. ENDURANCE: Hiyo wala si ndoto ni wazimu mtupu, kweli dada niamini.
15. DESIRÉE: (angry) Oh, nyamaza, funga mdomo wako Endurance!
16. GRANMA: Desirée. Omba msamaha mara moja. Siwezi kukubali lugha ya aina hiyo nyumbani kwangu hata kidogo.
17. DESIRÉE: (sarcastic) Samahani, kaka.
18. ENDURANCE: hapana omba samahani vizuri, la sivyo huendi.
19. DESIRÉE: Jamani ni ni kosa gani kubwa nilofanya? Siruhusiwi kuwa maisha yangu?

20. GRANMA: Sote tunaruhusiwa kuwa na maisha, ila tu tutimize jukumu letu kwa Mungu.
21. ENDURANCE: Hata siyo haki! Nani ataniandalia chai asubuhi?
22. DESIRÉE: Ni kama vile huwezi kujichemshia maziwa. Kwani wewe bado ni mtoto?
23. GRANMA: Tosha sasa, Desirée! Kupika sio kazi ya wavulana.
24. ENDURANCE: (sticking out tongue) Unaona? Errhhh!
25. DESIRÉE: (frustrated) Baadhi ya wapishi bora duniani ni wanaume.
26. ENDURANCE: Hah, lakini hao ni wapishi wa mahoteli makubwa sio wapishi wa kawaida.

27. DESIRÉE: (furious) Endurance! Kwa hivyo una maana kuwa wanaume ni watu waliojifunza upishi lakini wanawake ni wapishi wa kawaida tu?
28. GRANMA: Desirée. Nimesema mazungumzo hayo yametosh! iwapo Bella atakuja kunisaidia basi wewe unaweza kwenda kwa kina mwishoni mwa wiki.
29. DESIRE: (happy) Asante nyanya Linda!
30. GRANMA: lakini kwa sharti moja tu!
31. DESIRE: Lipi?
32. GRANMA: ni lazima umchukue Endurance uende nae. Tumeelewana?
33. ENDURANCE: (triumphant) NDIO!
34. DESIRE: groans

NARRATOR: Ni kipi ambacho Desirée angekisema zaidi? Labda mdogo wake atapata fursa ya kumuona kaka pacha wa Lorraine, Eric, jinsi anavyosaidia nyumbani kwao. Alimuona wakati Fulani akifua nguo. Lakini la muhimu zaidi lilikuwa ni kuweza kumuuliza Bi. Alice baadhi ya maswali kuhusiana na kifo cha mama yao. Kwa nini hakuna mtu alieyanusuru maisha yake?

35. **SFX:** Town ambience; traffic; bus; footsteps.

Baada ya safari ndefu kwa basi, Endurance na Desirée wamewasili katika mji wa Kentown. Mama yake Lorrain Bi. Alice, anawakaribisha ndani.

Scene 2 At home at Aunty Alice house

36. **ALICE:** (very warm)Hah! Desirée! na Endurance! Karibuni ndani! Lorraine na Eric wametoka kidogo. Watarudi sasa hivi. Je mngependa kunywa juisi ya maembe?

37. **SFX:** Door shuts. Footsteps on tiles

38. **DESIRÉE:** Mimi ninataka maji ya kunywa tu.

39. ENDURANCE: Mimi nitakunywa hiyo juisi ya maembe.
Baridi tafadhali!
40. DESIRÉE :(Hissing angrily) Endurance!
41. ALICE: (laughing) Kijana anajua anataka nini! Vipi au na
wewe nikuletee, Desirée? Usiogope sema
tu.!
42. DESIRÉE: Sawa nitakunywa. Asante.
43. ENDURANCE: (Sticking tongue out) Err. Unaniigiza!
44. DESIRÉE: Oh, hebu nyamaza!
45. **SFX:** Tinkling ice cubes in glasses
46. ALICE: (on mic) haya karibuni. Enhe mnaendeleaje?
47. DESIRÉE: (laughing) Salama tu. Ilikuwa vigumu kidogo
kupata ruhusa ya ya kuja huku!

48. ENDURANCE: Nyanya amebaki peke yake kwa hivyo ana kazi ya kuwatunza watoto wadogo wanne.
49. ALICE: Watoto wanne?
50. DESIRÉE: Ndio ni binamu zetu. Ni watoto wa mjomba wetu Blessing. Mkewe alifariki.
51. ALICE: (remembering) Oh nakumbuka! Ulikuwa msiba mkubwa. Kwa hivyo nyanya yenu aliwachukua wajukuu zake?. Sasa kuna hao watoto wanne, wewe, Endurance, na dadaenu Bella?
52. DESIRÉE: Ndio lakini Bella ameshaondoka nyumbani sasa anaishi na mpenzi wake kwa sababu nyumbani kuna heka heka nyingi. Anataka kuendelea na masomo. Lakini haishi mbali na sisi kwa hivyo amekuja kumsaidia nyanya wiki endi hii. Kuna kazi nyingi sana kwetu.
53. ENDURANCE: Ni kweli. Mimi huwa lazima niamke saa kumi na moja alfajiri kila siku kuchunga ng'ombe.

54. DESIRÉE: Ndio maana analala darasani.
55. ENDURANCE: (hissing angrily) hapana silali!
56. ALICE: Oh maskini! Lazima huwa unachoka sana.
Hivi una na miaka mingapi sasa?
57. ENDURANCE: Nina miaka13.
58. ALICE: Unasema kweli una miaka 13? Yaani huwezi kuasmini , Endurance, mimi ndie nilie mzalisha mama yako wakati alipokuzaa wewe! Pia nilimsaidia mama yako mara tu nduguyo mdogo Benedict alipozaliwa.
59. ENDURANCE: Na wakati huo ndio alipofariki mama.
60. ALICE: Ndio- ni wakati ambapo wote wawili walifariki.
61. DESIRÉE: Ni kitu gani kilichosababisha kifo chake?

62. ALICE: Nafikiri ni kwa ajili ya kuchoka. Mama yenu hakuwa na muda wa kupumzika wa kutosha kwa sababu alipata watoto mfululizo tangu alipoanza kuzaa akiwa na umri wa miaka 19. Alijaribu kutopata mtoto bada ya kuzaliwa wewe Endurance. Wewe ulikuwa mtoto wake wa tano.
63. ENDURANCE: Wa tano?
64. DESIRÉE: Ndio, Endurance. Mama aliavya mimba mara mbili kabla yaw ewe kuzaliwa. Lakini Aunty, kwa nini alikufa?
65. ALICE: Unajua. Uja uzito ni ya hatari wakati wote. Kusukuma mtoto wakati wa kujifungua ni hatua inayochokesha sana. Hatari zinazo weza kujitokeza ni kama vile mtoto kukwama, au umbo la mwanamke likiwa halina upana wa kutosha au hata kumwaga damu nyingi. Mama yako alipata matatizo ya mtoto kukwama kwa hali kama hiyo alihitaji kufanyiwa operesheni na bahati mbaya yeye alikuwa mbali mno na hospitali kuu ya Kentown.

66. **DESIRÉE:** Kwa hivyo haikuwezekana kuyanusuru maisha yake bila operesheni.
67. **ALICE:** La. haikuwezekena! Angalia – mama mja mzito anahitaji matibau ya afya kabla na baada ya kujifungua. Wakati wa kupima mimba mama huangaliwa shinikizo la damu yake, uzito na pia huangaliwa kama kuna dalili zozote zinazoweza kusababisha matatizo. Lakini mama yako hakufika kliniki hata mara moja kupimwa.
68. **ENDURANCE:** Kwa nini?
69. **ALICE:** Kentown ni mbali ni mji ambao uko kilomita 20 kilometres kutoka kwenu. Usafiri ni ghali mno ndio maana nimekuwa nahimiza kampeni kwa waziri ili afungue kliniki katika kijiji cha Mtelera. Kama tungefanikiwa kuwa na kliniki hiyo kabla mama yako...ha...oh..lakini (sighs), hakuna haja ya kujitamanisha. Nasikitika!
70. **SFX:** Front door slams

71. LORRAINE: (off mic) Halloo. Tumerudi! Des!
(greeting kisses)
72. ERIC: Vipi Des! Hujambo?
73. DESIRÉE: (shy) Sijambo Eric!.
74. ERIC: Na Endurance! Vipi Mambo!
75. **SFX:** Clap hands as they give each other “Big Five” greeting.
76. ENDURANCE: Poa Boss! Hebu nione hii? Rina? Ni nani huyu?
77. LORRAINE: Hii ni sauti mpya kutoka jamuhuri ya Kidepkrasi ya Kongo – anatesa!
78. ERIC: Pia unaweza kujiendeleza na Kifaransa ukimsikiliza!
79. DESIRÉE: (doubtful) Sawa.

80. LORRAINE: Des! Twende chumbani kwangu tukajifunze track ya kwanya tuone kama tunaweza kuishika halafu tutamuimbia Bongo.
81. DESIRÉE: Kwa KifaransaIn ? lakini mimi siwezi.
82. LORRAINE: Ni maneno matatu tu – “je t’aime”!
83. ERIC: (mimicking) Je t’aime – oooohhhh je t’aime oooooohhh , Endurance! Twende zetu tuwaache wasichana waimbe.
84. **SFX:** Eric and Endurance keep mimicking “Je t’aime – oooohhhh je t’aime oooooohhh !“ FADE UNDER
85. LORRAINE: (off mic) Saio hivyo nyinyi mnapiga kelele kama fisi! Sisi tunaweza kuimba! (on mic) Des! Bongo anatutarajia kesho saa sita mchana! Kazi yetu ikimfurahisha basi atayapendekeza majina yetu kwenye uchaguzi wa kuwafuta watu watakao shiriki kwenye mashindano ya pop idol katika mji wa Granville! Tujitahidi sana rafiki yangu!

SIG TUNE UP

OUTRO

Hadi hapo ndio tumefikia mwisho wa sehemu ya tatu katika kisa kwa jina Chini ya Miembe hadithi iliyotungwa na kuandikwa na Romie Singh. Mchezo huu wa Redio unaangazia jinsi matumizi bora ya mpango wa uzazi yanavyo weza kuboresha maisha. Uzazi kwa Mpango unawapa wanawake na wandani wao fursa ya kuamua wakati wa kupata mtoto. Usikose kujiunga nasi katika sehemu ya nne ambapo Desirée anagundua tembe chumbani kwa Lorraine na Eric nae anagundua kuwa anavutiwa na Desirée.

Kumbuka kuwa unaweza kuusikiliza tena mchezo huu au unaweza pia kumwambia rafiki yako juu ya mchezo huu wa kulisimua anuani ya mtandao wetu ni: dwworld.com au dwworld.com

Hadi wiki ijayo kwaheri.

END OF EPISODE THREE